KANISA LA WAADVENTISTA WA SABATO UNIONI YA KUSINI MWA TANZANIA

CHAMA CHA WACHUNGAJI/HUDUMA ZA MAOMBI

SIKU 100 ZA MAOMBI: MACHI 27 – JULAI 04, 2020

MADA: KUMWITA YESU KATIKA HITAJI LETU LA HARAKA

Limeandaliwa na: Frank M. Hasel – Mkurugenzi Msaidizi wa Taasisi ya Utafiti wa Kibiblia - GC

Mtafsiri: Mch. Herbert I. Nziku – Mratibu - Huduma za Maombi: STUM

Juma la Kumi na Tatu, Juni 19 – Juni 25, 2020

URITHI WA WEMA

Babu yangu, Franz Hasel, alikuwa ni mchungaji aliyewekewa mikono wa Kanisa la Waadventista wa Sabato nchini Ujerumani. Wakati wa Vita Kuu ya Pili ya Dunia, alilazimishwa kwenda jeshini kinyume na dhamiri yake. Kwa sababu babu yangu alitaka kuheshimu amri za Mungu, ikiwemo "Usiue," aliomba kuhudumu kwenye kitengo cha utabibu na alikataa kutumia silaha. Lakini ombi lake lilikataliwa. Badala yake, alipangwa katika kikosi kingine cha mstari wa mbele kama karani wa kikosi. Hata hivyo, azima yake ya kutoua aliichukulia kwa umakini mkubwa, kiasi kwamba alichukua bunduki ya mti (toy) kwa kipindi chote cha vita. Ingawa mara nyingi alifikiri kuwa angeweza kufa, Mungu alimlinda babu yangu kimuujiza mara kwa mara. Kisa chake chenye kutia moyo kilikuja kusomwa kwenye kitabu kiitwacho *A Thousand Shall Fall, (yaani Elfu Wataanguka)*

Babu yangu, kila mara alikuwa akitusimulia hadithi ambayo haimo kwenye kitabu cha *A Thousand Shall Fall*. Alipokuwa anatumika Urusi, kikosi chake kilipangiwa kukagua nyumba zote katika kila kijiji kilichotekwa na Wajerumani walipokuwa wanaivamia Urusi. Waliamriwa kuwatafuta wapiganaji wa waasi, waliojificha ndani ya nyumba na kuyashambulia majeshi ya Kijerumani yaliyokuwa yanasonga mbele. Waliambiwa kumpiga risasi mara moja na bila upendeleo kila mtu watakayemkuta amejificha.

Siku moja, Babu yangu alipokuwa akikagua nyumba moja kwa makini, alihisi kuwa kuna kitu sio cha kawaida. Alipoingia chumba fulani, kilikuwa kitupu, lakini bado, kilikuwa mwonekano kwamba kitu fulani kina mashaka. Alipoangalia kwenye uvungu wa kitanda, alimwona kijana akimtazama. Babu yangu alijua kuwa endapo angemtoa nje yule kijana, kwa vyo vyote vile angepigwa risasi. Macho yao yaligongana kwa muda wa kama nusu sekunde na ilionekana kama muda wa milele. Kisha Babu yangu aliinuka na kutoka nje ya kile chumba, na hakutoa taarifa juu ya kile alichoona. Alimhurumia yule kijana na kuunusuru uhai wake.

Majuma kadhaa baadaye, babu yangu alikuwa amepangiwa kulinda behewa la muhimu katika reli. Jukumu lake lilikuwa ni kuhakikisha kuwa mabehewa hayapigwi mabonu na wapiganaji wa waasi. Alikuwa akilinda peke yake wakati kikosi cha askari wapanda farasi cha jeshi la Warusi kiliposhambulia kuelekea kwake. Hakukuwa na njia yo yote ya kutoroka. Alikuwa tayari kwa kifo, akiamini kuwa kwa hakika wangemwua.

Kile kikosi kikamzunguka kwa haraka, lakini Babu yangu alishtuka alipoona uso wa kamanda aliyekuwa anawaongoza. Alikuwa ni yule kijana aliyomwona akiwa amejifucha kwenye uvungu wa kitanda katika ile nyumba. Ghafla wakatambuana. Yule kamada kijana akaielekeza bunduki yake kwa babu yangu na kumpa ishara kuonesha kuwa, "Ningeweza kukuua sasa hivi, lakini ulikuwa mwema kiasi cha kuokoa uhai wangu. Kwa hiyo nitayanusuru maisha yako!" Kisha akawaamuru watu wake waendelee na msafara wao. Maisha ya babu yangu, kwa mara nyingine tena, yaliokolewa kwa neema ya Mungu. Wema wa upendo kwa yule mtu na uaminifu wake kwa Mungu ulimrudia. Ninayo shukrani kubwa kwa maisha ya wema na kielelezo cha uaminifu na upendo wa wema aliouacha nyuma babu yangu. Urithi huu unaweza kuwa wetu pia.

Kuna kitu fulani cha pekee kuhusu *uaminifu.* Ingawa unaweza kuwa maarufu kidogo au tajiri kidogo, huwezi kuwa mwaminifu *kidogo.* Uaminifu una kitu cha peke kinachotaka umakini usiogawanyika. Ama wewe ni mwaminifu kwa asilimia 100 au sio mwaminifu. Ikiwa wewe ni mwaminifu kwa asilimia 95, wewe sio mwaminifu. Uaminifu unahitaji kujitoa kikamilifu. Mungu anahitaji uaminifu wetu kamili usiogawanyika, kujitoa kikamilifu.

Katika Agano la Kale tunasoma kisa cha Danieli, aliyetupwa kwenye tundu la simba kwa sababu hakutaka kuhafifisha imani yake kwa Mungu. Danieli alipojipambanua kuwa ni mwenye hakima, kiongozi mwenye kutegemewa na mfalme, adui zake wakawa na wivu na walitafuta njia za kumshitaki kwa matendo maovu. "lakini hawakuweza kuona sababu wala kosa; kwa maana alikuwa mwaminifu" (Danieli 6:4). Tumaini langu ni kuwa adui zetu (kama tunao) na rafiki zetu, na wote waliokuwa wakiyatazama maisha yetu katikati ya zahama ya COVID-19, watagundua ndani yetu maisha kama ya Danieli! Hebu tujulikane kama watu kwa wema halisi wa upendo tunaouonesha kwa wengine na hebu tuheshimiwe kwa uaminifu wetu katika mambo tunayofanya kila siku. Na kama Danieli, hebu tumtumaini Mungu atulinde tunapokuwa waaminifu kufanya mapenzi yake. Haijalishi siku za usoni zitakuwaje, hebu na tuwe wanaume na wanawake tulio wema kati Yesu na tulio waaminifu kwa Mungu na Neno lake.

MASWALI YA KUJIHOJI MOYONI

Unawezaje kuonesha matendo halisi ya urafiki kwa watu wanaokuzunguka? Ni katika maeneo gani unaona ni vigumu kuwa rafiki kwa wengine na kuwa mwaminifu kwa Mungu? Ni njia gani za pekee unazohitaji kukuza katika uaminifu wako? Danieli ni kielelezo cha namna uaminifu wa mtu mmoja kwa Mungu unavyoweza kushawishi ufalme mzima. Hali yako ya urafiki inawezaje kuwasaidia wengine waione tabia ya kweli ya Mungu na ni kwa namna gani uaminifu wako kwa Mungu unaweza kufungua milango ya kuonehsa uaminifu wake kwa wale wanaokuzunguka?

CHANGAMOTO ZA MOYONI

Inaweza kuwa rahisi kudai hadharani kuwa tuna uaminifu kwa Mungu kwa maneno na nyimbo. Hata hivyo, kila mara ni katika mambo madogo ya maisha – wakati hakuna mtu anayetazama, au hakuna mtu unayemfahamu anakutazama – ndipo uhalisi wa uaminifu wa mtu unapopimwa. Mwombe Mungu akusaidie kuona maeneo ya maisha yako yanayotakiwa kufanyiwa kazi. Mwombe Yesu aishi maisha yake ndani yako, na akupe uwezo wa kuchagua uaminifu unapokabiliwa na jaribu.

"Sio uthibitisho wenye hitimisho kwamba mtu ni Mkristo kwa sababu anaonesha furaha ya kiroho katika mazingira yasiyo ya kawaida. Utakatifu sio unyakuo: ni usalimishaji mzima kwa mapenzi ya Mungu; ni kuishi kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu; ni kufanya mapenzi ya baba yetu wa mbinguni; ni kumtumainia Mungu katika majaribu, gizani na kwenye nuru pia; ni kutembea kwa imani na sio kwa kuona; ni kumtegemea Mungu kwa ujasiri usio na maswali, na kupumzila pendono mwake." – Acts of the Apostles, p. 51

Mapendekezo ya aya za ziada za kusoma juma hili:

- Ellen White, *Christian Help Work*
- Frank M. Hasel, *Living for God: Reclaiming the Joy of Christian Virtue*

Siku ya 85, Jumamosi, Juni 19, 2020

USHUHUDA WA SIFA:

- Lovesky J., anasema, “Mungu aliliweka moyoni mwangu wazo kwamba niweze kuwashirikisha wengine ujumbe wa Siku 1000 za Maombi, na ndani ya siku moja, zaidi ya watu 500, walijiunga ili kupokea ujumbe kutoka kwangu kwa njia ya Whatsapp na Telegram. Tunaomba kila jioni saa mbili.”
- Tunaona Bwana akitoa baraka na hekima kwa viongozi wa kanisa lake na washiriki ulimwenguni kote namna ya kushughulikia changamoto za hili janga na zaidi ya hapo. Fedha, afya, kufungua makanisa, Mungu anafanya kazi katikati ya tufani!

MAMBO YA KUOMBEA

- **Ombea** uaminifu zaidi maishani mwako, na moyo ambao daima unaakisi wema wa Yesu.
- **Ombea** kituo cha mambo ya kiafya kiitwacho *Manna House*, nchini Uingereza, ambacho kinapanga kuendesha programu ya kuleta unafuu baada ya janga la COVID-19 na kuwafikia watu kwa njia ya ujumbe wa afya. Ombea wapate kibali cha serikali wanachokihitaji.
- **Ombea** Kituo cha Mafunzo kiitwacho 1000 Missionary Movement, kilichoko Kaskazini mwa Sumatra, pamoja na vituo vyote vya mafunzo za kimishonari, ili wapate njia za kuendeleza huduma zao, hata katika janga hili la COVID-19
- **Ombea** washiriki waliopoteza wapendwa wao katika janga hili, au kwa sababu zingine.

Siku ya 86, Jumamosi, Juni 20, 2020

AHADI YA TUMAINI

*"*Msifadhaike mioyoni mwenu; mnamwamini Mungu, niaminini na mimi. Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi; kama sivyo, ningaliwaambia; maana naenda kuwaandalia mahali. Basi mimi nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu; ili nilipo mimi, nanyi mwepo – Yohana 14:1-3

"Hatuna nyumba hapa; sisi ni wasafiri na wageni tu, tukipita kuelekea kwenye nchi iliyo bora, nchi ya kimbingu. Weka moyo wako katika mambo haya, na unapo fanya hivyo, Kristo atakuwa pale kando yako." – Life Sketches of Ellen G. White, p. 29

MASWALI YA KUJIHOJI MOYONI

Kwa sababu ya rehema ya Mungu, neema na wema wa upendo, tumepewa tumaini. Tumaini kwa ajili ya kesho iliyo bora, tumaini kwa ajili ya msamaha na ushindi dhidi ya dhambi, na tumaini kwa ajili ya uzima wa milele. Shetani na ulimwengu huu hutupatia sababu zisizo na idadi ili tuyakatie tamaa maisha, lakini katika Yesu, "ahadi zote za Mungu zilizopo katika yeye ni Ndiyo" (2 Kor. 1:20). Je! Utachagua kuzishikilia ahadi za tumaini ulizopewa katika neno la Mungu na kuthibitishwa kwako kwa damu ya Yesu? Je! Utamwomba akusaidie kudumisha macho yako katika tumaini la Kuja kwake Mara ya pili na uzima wa milele pamoja naye?

USHUHUDA WA SIFA

- Mtu ambaye hakutajwa jina, anasema, "Tulimwomba Mungu atupatie mahitaji kwa ajili ya kujenga kanisa, na alifanya kazi ndani ya moyo wa mfanya biashara tajiri, akatoa rasilimali zilizohitajika!"
- Idadi ya wagonjwa wa COVID-19 inapungua katika Ulaya na maeneo mengine duniani kote. Kasi ya watu kulazwa hospitalini inazidi kupungua wakati nchi nyingi zinafunguka tena huku zikizingatia kuepuka misongamano na taratibu zingine.

MAMBO YA KUOMBEA

- **Omba** Kwamba Yesu akupatie ufunuo mpya kwa ajili ya tumaini la utukufu ulilonalo katika yeye.
- **Ombea** uongofu wa wanafamilia yako, marafiki, wafanyakazi wenzako, na pia majina ya watu yaliyopelekwa kwenye timu ya Maombi ya Siku 100
- **Ombea** washiriki wanaochechemea kiroho, kimwili, au kiuchumi ili wadumu kuwa imara wawapo kwenye majaribu mbali mbali, watafuta msaada kwa Yesu.
- **Ombea** makanisa na huduma mbali mabali katika Konferensi ya Kusini mwa Uingereza. Omba wapate miujiza ya kifedha ili waanzishe makanisa na kukarabati majengo yaliyopo yaweze kuhudumia jamii zinazowazunguka.

Siku ya 87, Jumapili, Juni 21, 2020

AHADI YA FURAHA

*"*Matumaini yao wenye haki yatakuwa furaha" – Mithali 10:28a

"Roho inayothamini upendo wa Kristo imejaa uhuru, nuru, na furaha. Ndani ya roho hiyo hakuna fikra zilizogawanyika. Mtu kamili anamtamani Mungu. Haendi kwa wanadamu ili kujua wajibu wake, bali kwa Kristo, aliye chanzo cha hekima yote"– Reflecting Christ, p. 114

MASWALI YA KUJIHOJI MOYONI

Je! Umewahi kujisikia furaha ya Bwana? Furaha ya kuwa pamoja na Bwana, ya kushiriki pamoja naye kwa njia ya maombi na Neno lake? Unapopata mwonjo wa Yesu katika uzuri wake, mambo yote "ya kufurahisha" ambayo ulimwengu unayatoa hufifia kwa kukosa umuhimu. Yesu na mvuto wake usio na kifani; ataujaza moyo wako na furaha ambayo kiuhalisia sio ya ulimwengu huu! Je! Unatamani kupata furaha ya mbinguni? Furaha ya wokovu, furaha ya uaminifu, furaha ya mwafaka na kushirikiana na Mungu? Kwa nini usimwombe Mungu leo akupatie ladha ya furaha yake kwa kutumia muda zaidi pamoja na yeye katika maombi na tafakari ya Neno lake?

USHUHUDA WA SIFA

- Luninga iitwayo Novo Tempo (chini ya Hope Channel - Brazil) imejitoa kwa ajili ya uinjilisti saa 24 kwa siku 7 za juma. Juma moja kabla ya Pasaka ni wakati maalumu kwa ajili ya uinjilisti katia Divisheni ya Amerika ya Kusini. Makanisa yote yalipofungwa kwa ajili ya janga hili, viongozi waliomba. Waliamua kuendesha mkutano wa injili pamoja na Mwinjilisti Luís Gonçalves ambapo walipata maombi ya watu 30,256 wakihitaji kubatizwa! Hakika Mungu yupo tayari kutenda mambo yote pamoja kwa ajili ya wote wampendao Bwana!
- Mtu ambaye hakutajwa jina: anasema, "Katika masomo ya Siku 100 za Maombi nimetambua kuwa ninamhitaji zaidi Yesu kuliko mimi mwenyewe. Namsifu Mungu kwa upendo wake na neema kwangu!

MAMBO YA KUOMBEA

- **Ombea** moyo unaojazwa furaha ya mbinguni kila siku
- **Ombea** waumini wanaokabiliwa na majaribu mbali mbali kuhusu ushikaji wa Sabato. Omba ili uaminifu wao ung'ae katikati ya giza la changamoto na mateso
- **Ombea** Chuo cha Waadventista cha Naga View nchini Ufilipino kiendelee kuwa hai licha ya janga la COVID-19
- **Ombea** janga la VOVID-19 liishe

Siku ya 88, Jumatatu, Juni 22, 2020

AHADI YA UPENDO

*"*Bwana alinitokea zamani, akisema, Naam nimekupenda kwa upendo wa milele, ndiyo maana nimekuvuta kwa fadhili zangu.*"* – Yeremia 31:3

"Mpango ulikuwa umebuniwa ambapo neema ya ajabu na upendo wa Kristo vitadumu kufunuliwa kwa ulimwengu. Katika fidia isiyo na kikomo iliyolipwa na Mwana wa Mungu kumkomboa mwanadamu, upendo wa Mungu umedhihirishwa. Mpango huu wenye utukufu wa wokovu unapatikana na kutolewa ili kuuokoa ulimwengu mzima. Mwanadamu mwenye dhambi na aliyeanguka anaweza kukamilishwa katika Yesu kwa njia ya msamaha wa dhambi na haki ya Kristo" – Messages to Young People, p. 137

MASWALI YA KUJIHOJI MOYONI

Mungu ni upendo. Unapofungua ukweli huu na kuanza kuona yote anayofanya kwa njia ya lensi hii ya upendo mkamilifu, maisha yako yatabadilishwa na kuakisi upendo wa Mungu na kuwa mfereji wake. Kila ahadi ya Mungu ni ahadi iliyotokana na upendo. Mungu, kwa upendo wake, hutamani akufanye kuwa mtu wa upendo! Je! Umeruhusu upendo wa Mungu ufanye kazi yake ya kuyeyusha ubinafsi wote ndani ya moyo wako? Utamruhusu Yesu, kwa njia ya Neno lake, afafanue upya upendo wa kweli unajisikiaje, ukoje na unatendaje kazi? Je! Utakubaliana na mchakato wa kufanyika mtu wa upendo?

USHUHUDA WA SIFA

- Francisca A., anasema, "Siku 100 za Maombi zimenisaidia mimi na watoto wangu kuwa na desturi ya kuomba kila siku asubuhi na jioni. Ninamsifu Mungu kwa ajili ya muda huu wa amaombi. Rafiki wa binti yangu alikuja kututembelea naye akapata uzoefu huo pia. Alipokwenda nyumbani kwao aliishawishi familia yao wawe na maombi kila siku, jambo ambalo wanalifanya hadi sasa!"
- Mike alikuwa anahangaika sana wakati walipofungiwa ndani. Siku moja alipokuwa akitazama programu za luninga aligundua Hope Channel. "Ninahitaji Tumaini" alijisemea mwenyewe. Alianza kutazama masomo ya Biblia kwa mjadala pamoja na programu zingine zinazogusa moyo. Alitazama mfululizo mzima wa Danieli, na mfululizo mwingine wa Ufunuo. Kama matokeo wa kujifunza, aliutoa moyo wake kwa Yesu!

MAMBO YA KUOMBEA

- **Ombea** hali ya kuthamini, kupokea na kufanyia kazi kwa kina na kwa ukamilifu upendo wa Mungu maishani mwako.
- **Mwombee** Evangelina N., na wengine wengi wanaosumbuliwa na saratani na magonjwa mengine. Ombea uponyaji wao.
- **Ombea** washiriki wapya waliobatizwa na kujiunga na kanisa muda mfupi kabla au hata wakati wa jangala COVID-19. Omba kwamba ukosefu wa hali ya ushirika wa Kikristo na huduma za kanisa havitakatisha tamaa uamuzi wao wa kumfuata Kristo**.**
- **Ombea** Kanisa la Hamilton SDA nchini Kanada. Omba Mungu abariki njia za kiubunifu za huduma katika kituo chao kiitwacho 'Really Living Center' kinachotoa huduma kwa jamii, shule ya mapishi, mafuta ya bure, vinywaji laini, na mazoezi ya kupanda myamba iliyo ndani.

Siku ya 89, Jumanne, Juni 23, 2020

AHADI YA HEKIMA

*"*Lakini mtu wa kwenu akipungukiwa na hekima, na aombe dua kwa Mungu, awapaye wote, kwa ukarimu, wala hakemei; naye atapewa.*"* – Yakobo 1:5

"Mungu tunayemtumikia hawapendelei watu. Yeye aliyempatia Sulemani roho ya hekima ya utambuzi anatamani kuwapatia watoto wake baraka ile ile... Mbeba mzigo anapotamani hekima zaidi ya anavyotamani utajiri, mamlaka, au umaarufu, hatakatishwa matumaini. Mtu kama huyo atajifunza kutoka kwa Mwalimu Mkuu sio tu jambo gani la kufanya, bali jinsi ya kulifanya kwa namna itakayopata kibali cha Mungu." – Prophets and Kings, p. 31

MASWALI YA KUJIHOJI MOYONI

Yesu ni hekima. Muda wote anajua njia ipi ni ya hekima zaidi katika kutenda, ushauri wa hekima, njia ya hekima ya kusonga mbele. Maisha yanatuletea changamoto nyingi, huenda zinahusiana na taaluma yako, familia yako, huduma yako, daima tunahitaji la hekima ya Mungu. Msifu Mungu, yupo tayari kuwapatia hekima wote wanaoomba! Je! unatamani kubadilishana ujinga wa fikra zako na hekima itokayo kwa Mungu? Upo tayari kupokea ushauri wa Mungu, hata pale unapokuwa kinyume na "hekima" ya ulimwengu na mawazo yako? Je! Utaufungua moyo wako kupokea ushauri wa Yesu wenye hakima inayoongoza kwenye maisha ya haki na upendo?

USHUHUDA WA SIFA

- Enock C., anasema, "Hebu utukufu na sifa apewe Bwana. Wakati wa zuio, kama familia, kila siku tulikuwa tunajifunza kitabu cha Mwanzo kwa kina tukiongozwa na kijana wetu wa miaka 27. Ilikuwa ni baraka kubwa kutambua kuwa kitabu cha Mwanzo kimejaa masomo mengi. Sasa tumejenga utamaduni wa Kujifunza Bibilia kama familia!"
- Robert C., anasema, "Ilifunguliwa programu ya maombi ya upatanisho kwa juma zima kwa ajili ya mfululizo wa mikutano ya injili kwa njia ya mtandao niliyomaliza hivi karibuni katika Konferensi ya Arizona. Makumi ya watu walibatizwa makanisani, mtoni na kwenye mabwawa!"

MAMBO YA KUOMBEA

- **Omba** hekima ya Mungu ijulikane kwako unapotumia muda pamoja na Mungu
- **Ombea** makanisa, shule, na taasisi za Kiadventista wanapotafakari kwa maombi, na kwa uangalifu hatua za kufungua upya.
- **Ombea** Waadventista wakaa pweke, ili waweze kupata utimilifu katika Yesu, na kujipatia wenzi wacha Mungu
- **Ombea** Hospitali ya Kiadventista ya Tokyo, ambayo imekuwa ikihudumia jiji hilo kwa zaidi ya miaka 90. Tafadhali mwombe Mungu aibariki na kuikuza kazi yao ili watu wa Tokyo wapate uponyaji wa kimwili na kiroho.

Siku ya 90, Jumatano, Juni 24, 2020

AHADI YA NGUVU

*"*Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu*"* – Wafilipi 4:13

"Natamani wote wangetambua uwezekano uliopo na yumkini kwa ajili ya wote wanaomfanya Kristo kuwa utoshelevu wao na tumaini lao"– Letter 45, 1893, par. 33

MASWALI YA KUJIHOJI MOYONI

Mungu ana uwezo wote. Hakuna jambo lililo gumu, tata, au lisilowezekana kwake – Mwumbaji wa uhalisi wote. Huchagua kutumia uwezo wake kusaidia, kuponya, na kurejesha. Kwa sababu maneno yake ni nguvu na uhai, amri zake zote, maagizo, na maelekezo vinakuja kwetu pamoja na ahadi itakayotimizwa maishani mwetu kwa sharti la imani. Imani huitoa nguvu iliyoahidiwa kwa ajili ya kuishi kwa uaminifu. Je! Leo utachagua kuiamini nguvu ya Mungu inayoweza kupatikana kwako kwa imani? Utamwamini Yesu, Neno aliyefanyika mwili, ili kukupatia uwezo wa kufanya mapenzi yake? Je! Utashirikiana na Yesu kuishi maisha ya uponyaji, kusaidia, na kurejesha?

USHUHUDA WA SIFA

- Sister D., anasema, "Kwa miaka mingi nimekuwa nikimtia moyo kaka yangu kwenda kanisani. Na sasa, tunapoabudu kwa njia ya mtandao, huwa anajiunga nasi kila Sabato! Tafadhali omba kwamba aweze kutoa moyo wake kwa Bwana, na Mungu afungue njia kwa ajili yake kuingia kanisani."
- Gem C., anasema, "Tunamsifu Bwana kwa ajili ya viongozi wa maombi nchini Ufilipino ambao maisha yao yalibadilishwa nyakati za maombi. Mwanzoni, baadhi ya viongozi walikuwa wanasita kukubali wito wa kuwa viongozi wa maombi, lakini sasa wengi wamepata furaha nyingi katika imani. Kwa hakika, vipindi vya maombi kwa njia ya mtandao vimekuwa ndio chanzo cha nguvu zao wakati wa janga hili.

MAMBO YA KUOMBEA

- **Ombea** imani katika ahadi za Mungu kwamba atatupatia nguvu za kufanya mapenzi yake.
- **Ombea** ndoa zilizovunjika ziweze kuponywa, upatanisho ufanyike kati ya wenzi waliotengana, na kwa Yesu kuwa kiini cha ndoa ya kila mwumini.
- **Mwombee** dada T. toka Tanzania, anayeteseka kwa namna mbali mbali kwa sababu ya uamuzi wake wa kuwa Mwadventista wa Sabato.
- **Ombea** kituo kipya nchini Belarus, chenye huduma ya kiwanja cha michezo, na miundo mbinu ya kuhudumia watu wenye mahitaji maalumu, na mengine zaidi. Tafadhali mwombe Mungu abariki na kukuza huduma hii muhimu ya kiuinjilisti, na awasaidie wahudumu kuwatambulisha wageni kwa Mungu.

Siku ya 92, Alhamisi, Juni 25, 2020

AHADI YA UZIMA

“. . . Nazishuhudiza mbingu na nchi juu yenu hivi leo, kuwa nimekuwekea mbele yako uzima na mauti, baraka na laana; basi chagua uzima, ili uwe hai, wewe na uzao wako; kumpenda Bwana, Mungu wako, kuitii sauti yake, na kushikamana naye; kwani hiyo ndiyo uzima wako, na wingi wa siku zako; upate kukaa katika nchi Bwana aliyowaapia baba zako, Ibrahimu, na Isaka, na Yakobo, kuwa atawapa.*”* – Kumb. 30:19-20

“Mpaji wa uzima atawaamsha wakati wa ufufuo wa kwanza watu wake aliowanunua, na hadi wakati wa saa ile ya ushindi, wakati tarumbeta ya mwisho itakapolia na jeshi kubwa likinuka kwa ushindi wa milele, kila mtakatifu alalaye atalindwa kwa usalama na ataongozwa kama kito cha thamani, anayefahamika na Mungu kwa jina. Kwa nguvu ya Mwokozi iliyokuwa ndani yao walipokuwa hai na kwa sababu walikuwa washiriki wa asili ya Mungu, watafufuliwa kutoka kwa wafu.” – Maranatha, p. 300

MASWALI YA KUJIHOJI MOYONI

Ni ukweli wa kushangaza kiasi gani! Mungu, aliye chanzo cha uzima, anatamani kuwapatia wote wanaomwamini nguvu ya kuishi maisha ya upendo, uaminifu, na haki katika upande huu wa mbingu. Na sio hivyo tu, pia kwa furaha hutoa uzima wa milele kwa watoto wake, kwa ajili yao kuishi pamoja naye milele katika afya kamili, furaha, na mwafaka! Tumsifu yeye!

Je! Umeushikilia ukweli wa habari njema iletayo uzima, ibadilishayo maisha, na yenye kustawisha uhai inayopatikana kwako ndani ya Yesu? Je! Unasubiri ile siku ya ufufuo, wakati wote wanaomwamini watakapopokea mwili wa kutokufa ili wafurahie uzima wa milele pamoja na Mungu wetu wa thamani sana anayetupenda?

USHUHUDA WA SIFA

- Carme A., anasema, “Mimi sina mume, ni mama wa wavulana watatu, ambao ni wanafunzi, ninafanya kazi na ninajihusisha kwa nguvu katika huduma ndani ya kanisa letu. Licha ya mahitaji mengi ya muda wangu na uwezo, Mungu ananisaidia. Tumekuwa tukiendesha programu ya Maombi ya Siku 100 kwa karibu pamoja na watoto, vijana, na watu wazima kila siku. Vijana wanajihusisha sana, wakiomba na kuuliza maswali. Licha ya mahitaji ya kifedha ya shule, ninamsifu Mungu kwa kunifundisha sana na kunibariki sana katika wakati wa hili janga. Ninafurahia kufanya huduma!
- Tunamsifu Mungu kwani baadhi ya watendakazi wa utume kule Mashariki ya Kati, wanapata uhuisho wa nguvu za kiroho. Baadhi yao waliondolewa kwenye kusanyiko kwa sababu ya kukata tamaa na kukosa uamsho. Lakini kwa sababu ya maombi ya pamoja kwa njia ya mtandao katika Siku 100 za Maombi, wanatamani kuwa sehemu ya kanisa tena.

MAMBO YA KUOMBEA

- **Ombea** tupate uzima tele aliotuahidi Yesu.
- **Ombea** wahamiaji Waadventista wote na watu wote wanaoishi kwa vibali, ambao kwa sababu ya hadhi zao kisheria, hawawezi kupata usaidizi wa serikali wakati wa janga hili. Ombea waweze kupata mahitaji ya muhimu ya maisha.
- **Ombea** Waadventista wote na wasio Waadventista waliopata maambukizi ya COVID-19.
- **Ombea** shule ya Rostok nchini Urusi, inayohudumia watoto wenye mahitaji maalum, ikiwapatia mtaala wenye kiini katika upendo wa Kristo, unaowaletea furaha watoto na wazazi pia. Tafadhali omba kwa ajili ya baraka za Mungu kwa ajili ya huduma hii muhimu na wafanya kazi wake, wanafunzi, na wazazi.